MAANDISHI YA
TANGAZO LA MKUTANO WA KIMATAIFA

# NI WAPI AHLU SUNNA WA JAMAA

## ANGAZO NA UFAFANUZI WA MFUMO WA AHLU SUNNA WA JAMAA[(1)] KIITIKADI NA UFAHAMU WA DINI NA KITABIYA, NA ATHARI YA KUPONDOKA KUTOKANA NA MFUMO HUO JUU YA HALI TUNAYOISHI.

### KWA JINA LA ALLAH MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU

KILA JINSI YA SIFA NJEMA NI ZA ALLAH BWANA WA VIUMBE WOTE, REHMA NA AMANI ZIWE JUU YA BWANA WETU MUHAMMAD NA JAMAA ZAKE NA SWAHABA WAKE WOTE, BAADA YA HAYO:

USIKU WA SIKU YA ALHAMISI TAREHE ISHIRINI NA MOJA YA DHUL-HIJJAH, MWAKA WA ELFU MOJA NA MIA NNE NA THALATHINI NA SABA SAWA NA TAREHE ISHIRINI NA TANO YA AUGUST MWAKA WA ELFU MBILI NA KUMI NA SITA MILADIYA, TUKIWA KATIKA MAJARIBIO YA VIKUNDI VYA KIKHAWARIJ YA KUIBA JINA TUKUFU LA “AHLU SUNNA WA JAMAA” PAMOJA NA WALIOTOKA KWENYE DINI WANAOTUMIWA MATENDO YAO YA MAKOSA KUCHAFULIWA TASWIRA YA DINI YA KIISLAMU, KULIFANYIKA MKUTANO WA KIMATAIFA WA WANAVYUONI WA KIISLAMU, IKIWA NI KATIKA KUHUISHA UKUMBUSHO WA SHEIKH SHAHIDI MTUKUFU RAISI AHMAD HAAJ QADIYROF (ALLAH AMREHEMU) KWA ANUWANI YA “NI WAPI AHLU SUNNA WA JAMAA? ANGAZO NA UFAFANUZI WA MFUMO WA AHLU SUNNA WA JAMAA KIITIKADI NA UFAHAMU WA DINI NA KITABIYA, NA ATHARI YA KUPONDOKA KUTOKANA NA MFUMO HUO JUU YA HALI TUNAYOISHI” KWA HISANI NJEMA YA MTUKUFU RAISI RAMADHAN AHMAD QADIYROF (ALLAH AMUHIFADHI) NA KUHUDHURIA KWA HALI YA JUU KWA MTUKUFU IMAAM NA SHEIKH MKUBWA WA AZHAR, NA MAMUFTI, NA ZAIDI YA WANAVYUONI MIA MBILI KUTOKANA NA WANAVYUONI WA KIISLAMU, KUTOKA SEHEMU TAFAUTI ULIMWENGUNI.

NA MKUTANO ULIMALIZIKA KWA YAFUATAYO:

- KUTEGEMEA KILMA CHA MTUKUFU IMAAM NA SHEIKH MKUBWA WA AZHAR KAMA MKATABA WA KIMSINGI WA MKUTANO HUWO.
- AHLU SUNNA WA JAMAA NI ASHAIRAH NA MATURIYDIYAH[(2)] KWENYE ITIKADI “NA KATI YAO NI AHLU HADITH WATEGEMEZAJI[(3)]” NA WFUASI WA MADHEHEBU MANNE YA HANAFIYAH NA MALIKIYAH NA SHAFIIYAH NA HANABILAH KWENYE FIQHI, NA WATU WA TASWAWUF SAFI KWENYE ELIMU NA TABIYA NA KUJITAKASA KWA MFUMO WA BWANA WA POTE HILO IMAAM AL-JUNAIYD NA WALIOKWENDA MWENDO WAKE KUTOKANA NA MAIMAAM WA UONGOFU, NAO NI MFUMO AMBAO UNAHESHIMU ELIMU ZINAZOTUMIKYIA WAHYI, NA UNAOWEKA WAZI KIKWELI MIELEKEO YA DINI HINI NA MAKUSUDIO YAKE KATIKA KULINDA NAFSI NA AKILI, NA KULINDA DINI KUTOKANA NA KUPOTOLEWA NA KUCHEZEWA, NA KULINDA MALI NA HISHMA, NA KULINDA JENGO LA TABIYA TUKUFU.

(1) MKUSANYIKO MKUBWA WA WAISLAMU WAFUASI WA MWENDO WA MTUME S.A.W.
(2) WAFUASI WA ITIKADI YA IMAAM AL-ASHARIY NA IMAAM AL-MATURIDIY.
(3) WALE WANAOMTEGEMEZEA MWENYEWE ALLAH MAANA YA SIFA ZAKE ZISIZO NA UWAZI.

▪ QURANI IMEZUNGUKWA NA NGOME ITOKAMANAYO NA ELIMU ZINAZOITUMIKIYA, ZINAZOSAIDIYA KUZINDUA MAANA YAKE, NA KUFIKIA MAKUSUDIO NA MALENGO YAKE YANAYOFIKISHA KWA ALLAH, NA KUTOWA ELIMU ZILIZOWEKWA NDANI YAKE, NA KUZIGEUZA AYAH ZAKE KUWA UHAI NA TAMADUNI, NA ADABU NA FANI NA TABIYA NA REHMA NA RAHA, NA KUAMINI NA KUIMARISHA, NA KUENEZA AMANI NA USALAMA ULIMWENGUNI, MPAKA JAMII NA TAMADUNI ZENGINE ZIONE WAZI KUWA DINI HINI NI REHMA KWA VIUMBE WOTE, NA NI NJEMA DUNIYANI NA AKHERA.

▪ MFUMO WA AHLU SUNNA WA JAMAA NDIO MFUMO NYETI NA WA SAWA UNAOKUSANYA ZAIDI WAISLAMU, NA ULIODHIBITIKA ZAIDI, NA NDIO WENYE UPELELEZI ZAIDI KATIKA KUCHAGUWA VITABU VYA KIELIMU NA MIFUMO YA KUSOMESHA AMBAYO YANAELEZEA SAWA NJIYA YA AKILI YA MUISLAMU KATIKA KUFAHAMU SHARIA TUKUFU, NA KUELEWA HALI ILIVYO NA UTATA WAKE, NA KUFUNGAMANISHA VYEMA KATI YAKE.

▪ MADRASA HIZO ZA KIELIMU ZINAZOWAKILISHA AHLU SUNNA WA JAMAA ZIMEJIPOTOLEYA KUPITIYA KARNE NYENGI KUTOWA MALAKI YA WANAVYUONI NA WALIOKHITIMU, AMBAWO WALIENEYA PAMBIZONI MWA DUNIYA KUTOKA SERBIYA MPAKA NAIJERIYA, NA KUTOKA TWANJA MPAKA JAKARTA, WAKATAWALA VYEO NA MADARAKA TAFAUTI, PAMOJA NA UMUFTI NA UKADHI NA KUSOMESHA NA UHUBIRI, IKAENEYA KWA AJILI YAO AMANI KWENYE JAMII HIZO, NA WAKAZIMA MOTO WA FITNA NA VITA, NA ZIKATULIA KWA AJILI YAO NCHI HIZO, NA IKAENYEKA KWA AJILI YAO ELIMU NA UELEWA SWAHIHI.

▪ AHLU SUNNA WA JAMAA WALISALIA WAKITEGEYA KILA FIKRA POTOFU, NA WAKITEGESHEYA MAKALA YA VIPOTE NA UFAHAMU WAO, NA WAKIZISMAMISHIA MIZANI ZA ELIMU NA UKOSOWAJI NA UPELELEZI, NA WAKIONESHA WAZI KUJITOLEYA NA UKAKAMAVU KATIKA KUPAMBANA NA SURA ZOTE ZA UPOTOFU, NA WAKITUMIA VIFAYA MADHUBUTI VYA ELIMU KATIKA KUCHAMBUWA NA KUWEKA SAWA, HIVO KILA UNAPOPATA NISHATI MFUMO WAO WA KIELIMU NDIPO YANAPOPUNGUWA MAWIMBI YA UPOTOFU, NA HUSIMAMA WIMA MAMBO YA UMMA NA KUWEZA KUMAKINIKA NA KULEKEYA KWENYE KUTENGEZA UTAMADUNI, NDIPO KUKAPATIKANA MABINGWA KUTOKANA NA WANAVYUONI WA KIISLAMU, AMBAO WALICHANGIA KWENYE ELIMU ZA JABR NA HISABU, NA ELIMU ZA HANDASA ZA UKAGUZI, NA WIZANI TAFAUTI, NA TIBA NA MAGONJWA NA MADAWA, NA ELIMU ZA HAYAWANI NA MIMEYA, NA ELIMU ZA ANGA NYOTA NA MAZINGIRA, NA ELIMU ZA SAUTI NA VYA KUONESHA, NA VISIOKUWA HIZO KUTOKANA NA ELIMU, NA ZOTE HIZO NI MATUNDA YA MFUMO WA AHLU SUNNA WA JAMAA AMBAZO HAZIKANUSHIKI.

▪ IMEKARIRI KUPITIYA ZAMA ZILIZOTANGULIYA KUVUMA MAWIMBI YA FIKRA POTOFU INAYOJIGONGA, INAYODAI KUNASIBIANA NA WAHYI MTUKUFU, NA INAYOPINGANA NA MFUMO SWAHIHI WA KIELIMU NA KUTAKA KUUVUNJA, NA INAYOTINGISHA AMANI YA WATU NA UTULIVU WAO, NA YALIKUWA MWANZO WA MAWIMBI HAYO YA UPOTEVU NA MADHARA, NI MAKHAWARIJ WA ZAMANI, KUFIKIA MAKHAWARIJ WA ZAMA ZA SASA KUTOKANA NA WANAODAI KUWA SALAFI WAKUFURISHAJI, NA DAISH NA WANAOKWENDA NA MFUMO WAO KUTOKANA NA MIKAO MIPOTOFU AMBAYO INAZINGATIWA KITU KINACHOWAGAWANYA PAMOJA NI UPOTOSHAJI SANA NA UDANGANYIFU BATILI,

NA UFAFANUZI USIO WA KIELIMU WA DINI, ULIOZALISHA UFAHAMU MWINGI MAKOSA UNAOGONGANA, NA MAELEZO BATILI AMBAYO YAMEZAA UKUFURISHAJI NA UBOMOWAJI, NA UMWAGAJI WA DAMU NA UHARIBIFU, NA KUCHAFUWA JINA LA UISLAMU, NA KUSABABISHA KUPIGWA VITA NA KUFANYIWA UADUWI, JAMBO AMBALO LILIWALAZIMISHA KUJITOLEYA WAADILIFU KATI YA WALIOIBEBA DINI HINI NYENYEKEVU KUWEZA KUITETEYA NA YOTE HAYO KUSWADIKISHA NENO LAKE S.A.W. KATIKA HADITHI SWAHIHI: " WATAICHUKUWA HINI ELIMU [DINI] WAADILIFU KATIKA KILA WATAKAOKUJA, WATAKAOITETEYA KUTOKANA NA UPOTOFU WA WENYE KUZIDISHA, NA UDANGANYIFU WA WENYE KUHARIBU NA UFAFANUZI WA WAJINGA ".

- MKUTANO HUNU UMEKUJA ILI KWA UWEZO WA ALLAH UWE CHANZO CHA MABADILIKO YALIOBARIKIWA YA KUREKIBISHA UPOTOFU MKUBWA NA HATARI ULIOVAMIYA UFAHAMU WA "AHLU SUNNA WA JAMAA" KUFUATIYA MAJARIBIO YA WAPOTOFU KULIIBA JINA HILI TUKUFU NA KUJIHUSISHA NALO WAO, NA KUWATOWA WENYEWE NDANI YAKE, NA HAYO NI KWA KUPITIYA KUFANYISHA KAZI MFUMO WA KIELIMU MADHUBUTI WA KIASILI ULIOSHKILIWA NA VYUO VYETU VIKUBWA VINAVYOTAMBULIKA KAMA VIGUZO VYA USALAMA KATIKA KUFETUWA BWAGIZO ZA KUKUFURISHA NA UPOTOFU, NA KUPITIYA KUTUMANA JUMBE ZA USALAMA NA HURUMA NA AMANI KWA VIUMBE WOTE, MPAKA IRUDI MIJI YETU YOTE KWA UWEZO WA ALLAH KUWA MAJUKWAA YA MUANGAZA, NA TIMBUKO ZA UONGOFU.

NA PIYA MKUTANO ULIMALIZIKA NA MAAGIZO KADHAA:

1. KUASISI KITUO CHA TELEVISHENI NCHINI URUSI KITAKACHOFIKISHA TASWIRA YA UISLAMU KWA WANANCHI NA KITAKACHOPIGA VITA UPOTOFU NA UGAIDI.

2. VYUO VIKUBWA VYA ELIMU VIRUDI KUJIELEWA NA KUELEWA TAREKHE YAKE NA MIFUMO YA ASILI YA KUSOMESHA YENYE MASHINA, NA KURUDI KUSOMESHA MIZUNGUKO YA ELIMU YALIYOKAMILIKA, YANAYOTENGEZA WANAVYUONI WANAOWEZA KUONGOZA, NA KUCHAMBUWA MAJANGA YA UPOTOFU WA KIFIKRA, NA KUENEZA ELIMU NA AMANI, NA KUHIFADHI MIJI.

3. DHARURA YA KUCHUNGA NA KUYACHUKULIYA HAMU MITANDAO YA MAASILIANO YA KIJAMII, NA KUHUSISHA NGUVU NA UJUZI UNAOLAZIMU KUWEKO HADHIR KATIKA MITANDAO HAYO KWA NGUVU NA KIUHAKIKA.

4. KUINUA KIWANGO CHA KUFANYIA HAMU NA KUCHUNGA KUSOMESHA ELIMU ZOTE ZA KIISLAMU, HASA HASA ELIMU YA USUL-FIQHI NA TAWHIDI ILI KUDHIBITI UPELELEZI NA KUSWAHIHISHA FIKRA NA KUCHAMBUWA MAKALA YA UKUFURISHAJI NA WAPINGADINI.

5. KUASISIWA KWA KITUO CHA KIELIMU KWENYE JAMUHURI ASILI YA SHISHANI ILI KUTEGEYA NA KUSOMA VIPOTE VYA KISASA NA UFAHAMU WAKE, NA KUTENGEZWE MKUSANYIKO WA MAELEZO UNAOAMINIKA UTAKAOSAIDIYA KUCHAMBUWA NA KUKOSOWA KIELIMU FIKRA POTOFU NA MAKALA YAKE, NA WALIOKUTANA WAMEPENDEKEZA KITUO HICHO KIWE NA JINA (**TABSWIIR**).

6. DHARURA YA KUINUWA KIWANGO CHA KUSHIRIKIYANA KATI YA TAASISI ZA KIELIMU ZA KIASILI KAMA AL-AZHAR TUKUFU, NA AL-QARAWIYN NA AL-ZAYTUNAH, NA VITUO VYA ELIMU NA UTAFITI KATI YAKE NA TAASISI ZA KIDINI NA KIELIMU NDANI YA MUUNGANO WA URUSI.

7. DHARURA YA KUFUNGULIWA KWA (MAJUKWAA YA KUSOMESHA) KUSOMESHA MBALI KWA MBALI ILI KUENEZA ELIMU SALAMA, KWANI MAJUKWAA HAYO YANAWAHUDUMIYA VYEMA WANAOTAKA ELIMU NA MAARIFA KUTOKANA NA WALE WANAOZUWILIWA NA KAZI ZAO KUJIUNGA NA MASOMO YA KIMPANGILIO.

8. KUZINASIHI SEREKALI JUU YA DHARURA YA KUZISAIDIYA TAASISI ZA KIDINI NA VITUO VILIVOSIMAMA WIMA KWENYE MIFUMO WA KATIKATI ULIOLINGANA, NA KUHADHARISHA JUU YA HATARI YA ZINAVOFANYA BAADHI YA SEREKALI KUCHEZA NA SIYASA ZA KUPIMANA NGUVU NA KUPIGANISHA UHUBIRI WA KIDINI, NA KUWA HILO HALIZAI ILA BABAIKO ZAIDI NDANI YA JAMII, NA KUBOMOWA JENGO LAKE.

9. MKUTANO UNAZINASIHI SEREKALI KUBUNI KANUNI ZINAZOKOSOWA KUENEZA CHUKI NA KUCHOCHEA FITNA NA KUPIGANA NDANI KWA NDANI NA KUZIKOSEA TAASISI ZA KIDINI.

10. WALIOSHIRIKI WANAZINASIHI TAASISI KUBWA ZA AHLU SUNNA, KAMA AZHAR NA MFANO WAKE, KUPEYANA NAFASI ZA KIMASOMO KWA WAISLAMU WANAOPENDA KUSOMA ELIMU ZA KISHARIYA NCHINI URUSI.

11. WALIOSHIRIKI WANAUSIA KUFANYIKA MKUTANO HUNU MUHIMU KILA BAADA MUDA, ILI KUTUMIKIYA MALENGO HAYA MAKUBWA, NA KUFUATILIYA MISUKOSUKO YATAKAYOJITOKEZA UPYA NA KUPAMBANA NAYO.

12. KUBUNI KAMATI ILI KUFUWATILIYA KUTEKELEZWA MATOKEO NA NASAHA ZILIOMO NDANI YA TANGAZO HILI.

NA WALIOSHIRIKI WOTE WAMETANGULIZA KWA MTUKUFU RAISI RAMADHAN AHMAD QADIYROF SHUKURANI KUBWA JUU YA JUHUDI ZAKE ZILIZOBARIKIWA KATIKA KUTUMIKIYA QURANI TUKUFU NA SUNNA TAKATIFU, NA WAKAMUOMBEYA TAWFIQ KUENDELEA NA MWENDO WA BABA YAKE ALIYEKUFA SHAHIDI SHEIKH AL-HAAJ AHMAD QADIYROF KATIKA KUTUMIKIYA UISLAMU NA UBINADAMU, NA KUTETEYA ITIKADI YA AHLU SUNNA WA JAMAA, HUKU WAKIINUWA MIKONO YA UNYENYEKEVU KWA MUUMBA ALIYETUKUKA AMFINIKE MAREHEMU KWA HURUMA NA RADHI NA AMPOKEE VYEMA PEPONI, NA AIHIFADHI SHISHANI NA AIDUMISHE SALAMA NA AMANI NA KUENDELEYA NA UFANISI.

KAMA VILE VILE WALIOSHIRIKI WALILEKEZA SHUKRANI KWA AFISI YA RAISI KWA USHIRIKIANO WAO MWEMA NA WASIMAMIZI, NA KISANDUKU CHA MAMBO YA KHERI CHA JIMBO KWA JINA LA SHEIKH SHAHIDI AHMAD QADIYROF, NA TAASISI YA MAMBO YA KHERI YA KUSAIDIYA TAMADUNI ZA KIISLAMU NA ELIMU NA KUSOMESHA, NA TAASISI YA TWABAH NA NDUGU WENGINE WALIOSHIRIKI KATIKA KUPANGILIYA MKUTANO HUNU.

NA REHMA ZA ALLAH NA AMANI ZIWE JUU YA MSIMAMIZI NA BWANA WETU MUHAMMAD, NA JUU YA JAMAA ZAKE NA SWAHABA ZAKE WOTE.

IMETOLESHWA SHISHAN, GROZNI, 24 DHUL-QAADAH 1437H, 27 AUGUST 2016